**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

SOMO LA PILI KATIKA

# "Tuijuwe njiya ya wokovu"

## KWA KUJIFUNZA NA KUTII NENO LA MUNGU KWA KUTARAJIA UZIMA WA MILELE

**Utangulizi**

*Mpendwa katika Kristo, ufuatao ni mfululizo wa masomo manane ambayo imeandaliwa kwa wakristo walio na nia ya kujuwa mambo ya muhimu kuhusu wokovu (kuufikiya na kuulinda) kwa nia ya kuepuka maangamizi ya milele inayotarajiwa kwa wale wasiojali neema kubwa Mungu alitupa kwa njiya ya Yesu Kristo.*

*Masomo haya yana mada zifuatazo:*
Somo la 1: Maisha bila Kristo
Somo la 2: Wokovu kwa njiya ya Kristo
Somo la 3: Mamlaka ya Kristo
Somo la 4: Imani katika Kristo
Somo la 5: Toba kwa jina la Kristo
Somo la 6: Ubatizo katika Kristo
Somo la 7: Kanisa la Kristo
Somo la 8: Maisha mapya katika Kristo

*"Na Filipo aliendа mahali alipo na kumsikia yule mtu anasoma kitabu cha nabii Isaya. Filipo akamwuliza, "Je, unaelewa maneno hayo unayoyasoma?" Yule towashi akasema, "Nitawezaje kuelewa pasipo mtu kunifafanulia?" Hivyo akamsihi Filipo ili apande na kuketi pamoja naye"*
(Mdo. 8:30-31).

*"Hivyo kwa mwaka mzima Barnaba na Sauli wakakutana na kanisa na kufundisha idadi kubwa ya watu. Ilikuwa ni katika kanisa la Antiokia kwa mara ya kwanza wanafunzi waliitwa 'Wakristo.'"*(Mdo. 11:26).

*"Lakini baadhi yao kwa ukaidi walipokataa kuamini na kukashifu ujumbe wake mbele ya umati wa watu, Paulo aliachana nao, akawachukua wanafunzi na kuhojiana nao kila siku katika darasa la mtu mmoja aitwaye Tirano"*(Mdo 19:9).

*"Watu hawa walikuwa wema kuliko wale wa Tesalonika, kwa sababu walipokea Neno kwa nia iliyokuwa tayari kabisa, wakatafuta Maandiko kila siku kujuwa hakika ya maneno yale (waliofunzwa)"*
(Mdo. 17:11).

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

*Mungu akubariki na kukuumbiya imani safi, juhudi na moyo wa utiifu kwa haya unayoyasoma.*

# **Somo la pili:** Wokovu kwa njia ya Kristo tu.

## Kristo ametolewa ili kutuokowa toka dhambini

Hali ya mtu katika dhambi itakuwa yenye kusikitisha ikiwa Mungu hangelikuwa na upendo mkubwa kwa mwanadamu. Kwa hiyo inaeleweka kwamba upendo wa Mungu utafanya kuweko na njia ya kuwaokoa watu kutoka utumwa, nguvu, hatia na matokeo ya dhambi, wakigeuzwa kutoka njia ya uharibifu wa milele na kuwaongoza kwenye njia ya uzima wa milele. Mpango huo wa Mungu ni Injili – " *Mimi siionei haya Injili ya Kristo kwa maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwanza kwa Myahudi na kwa Myunani pia"* (Warumi 1:16). Yoyote ambayo Mungu alipangilia inayohusu kusamehewa dhambi na wokovu, imefunuliwa yote wazi katika Injili, au "habari njema" ya Yesu Kristo.

Injili ndio uwezo Mungu anaotumiya kwa kuokowa watu kwa sababu inaeleza wazi kuhusu Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu na Mwokozi wa ulimwengu. Mada kuu ya Injili ni upendo wa ajabu wa Mungu alionyesha kwa kutoa zawadi kubwa sana, yaani Kristo, aliyehukumiwa kufa msalabani hapo Kalvari ambako alimwaga damu yake ili aziondowe dhambi za watu. "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele*" (Yohana 3: 16). "*Lakini Mungu anaudhihirisha upendo Wake kwetu kwamba: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu. Basi, kwa kuwa sasa tumehesabiwa haki kwa damu Yake, si zaidi sana tutaokolewa kutoka katika ghadhabu ya Mungu kwa Yeye!*" (Warumi 5:8-9.). "*Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu akimjia akasema, 'Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!"* (Yohana 1 : 29). "*Lakini Mimi, nikiinuliwa kutoka katika nchi, nitawavuta watu wote waje Kwangu*". Yesu aliyasema haya akionyesha ni kifo gani atakachokufa. (Yohana 12:32,33)..". "*Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake, juu ya mti, ili kwamba, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tupate kuishi katika haki. Kwa kupigwa kwake, ninyi mmeponywa"* (1 Petro 2:24). Soma tena Mathayo 27:29-50, Marko 15:15-38, Luka 23:27-46, Yohana 19:13-37.

## Sadaka za kuteketezwa na zingine za Agano la kale hazifai tena kwa wakristo

Sadaka za kuteketezwa zilizotolewa na Wayahudi chini ya Sheria ya Agano la Kale, ilikuwa ni kivuli cha sadaka ya Yesu juu ya msalaba. Damu ya dhabihu hizi

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

haikuwa na uwezo wa kuondoa dhambi (Waebrania 10:4). Hata hivyo, damu ni muhimu katika mpango wa Mungu kwa ajili ya ukombozi (Waebrania 9:22). Damu pekee iliyo na uwezo wa kuokowa watu na dhambi zao ni ile ya Yesu Kristo kwa kuwa hakuwa na dhambi na kwamba sadaka yake ilikuwa kamililifu, takatifu (Waebrania 4:15, 5:8-9, 1 Petro 1:18-19; 2:21-22).
Kwa kuwa Yesu Kristo ndiye Biblia inalenga kutujulisha tangu mwanzo hadi mwisho, na kufa pia kufufuka kwake ndiyo mada kuu ya Injili, ni rahisi kuona ni kwa nini Mtume Paulo alijumlisha ujumbe wake kwa kusema « *Kwa kuwa niliamua kutokujua kitu cho chote wakati nikiwa nanyi isipokuwa Yesu Kristo, naye amesulibiwa msalabani* » (1 Wakorintho 2:2). Hata hivyo, ni lazima tusisahau kwamba kifo cha Yesu Kristo msalabani kingekuwa bila maana kama hakufaulu kushinda mauti kwa njia ya ufufuo wake (1 Wakorintho 15:14-20, Warumi 4:25). Kwa hiyo, nguvu za Injili kwa ajili ya wokovu huelekeya kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo. Soma 1 Wakorintho 15:1-4. Wengi wa wale ambao wanadaiwa kwamba ni mitume wa kuaminika sana, manabii maarufu waliounda makundi fulani za dini, hakuna hata mumoja aliyewahi kusikika kwamba amefufuka na kusema tena atarudi. Kwa hiyo, wakristo wana haki ya kuzingatia imani yao katika Kristo Bwana wao bila kumchanganya na desturi za wanadamu pamoja na madhehebu. Wokovu ni kupitiya Yeye tu.

Sasa, tunataka kuona maelezo mbalimbali iliyotolewa katika Injili kuhusu suala la watu kuokolewa na Bwana pia Mwokozi Yesu Kristo kutokana na dhambi zao. Lakini katika somo hili, tueleze kwa ufupi kila hali na neno linaloambatana na wokovu yakiwa ni ukombozi, kuhesabiwa haki, kupatanishwa na Mungu, kusamehewa dhambi, kusafishwa na kuponywa roho.

**1.Wokovu.**
Mtu bila shaka amepotea katika dhambi (kumbuka somo la kwanza) ; hivyo basi, ana haja ya kuokolewa. Yesu amekuwa wa pekee kwa kutimiza hayo mapenzi ya Mungu na wokovu wapatikana kwake tu. "*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hakuna Jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo*" (Matendo 4:12). "*Naye atamzaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, kwa maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka katika dhambi zao*" (Mathayo 1:21). "*Kwa maana Mwana wa Adamu amekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea"* (Luka 19:10). "*Lakini twamwona Yesu, aliyefanywa chini kidogo kuliko malaika, sasa akiwa amevikwa taji ya utukufu na heshima kwa sababu alistahimili mauti, ili kwamba kwa neema ya Mungu apate kuonja mauti kwa ajili ya kila mtu. Ili kuwaleta wana wengi katika utukufu, ilimpendeza Mungu, kwa ajili Yake na kwa kupitia Yeye kila kitu kilichopo, kumkamilisha mwanzilishi wa wokovu wao kwa njia ya mateso*" (Waebrania 2:9,10).

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

Soma tena Waebrania 7:25, 1 Petro 2:25, 1 Timotheo 1:15, Warumi 8:1.

**2. Ukombozi**
Mwenye dhambi ni mtumwa wa dhambi na wa Shetani (Warumi 6:16). Hawezi kufanya kitu peke yake kujikwamua kwenye huo utumwa. Bei iliyolipwa kwa fidia (rançon) yake ni damu ya thamani ya Yesu iliyomwagika msalabani, "*ambaye katika yeye tuna ukombozi kwa njia ya damu yake …*" (Wakolosai 1:14). Soma Matendo 20:28, 1 Wakorintho 1:30, Waebrania 6:20, 9:12. Kwa kumkomboa mwanadamu toka utumwa wa dhambi, Yesu ameharibu nguvu na kazi za Shetani. "*Yeye atendaye dhambi ni wa Ibilisi, kwa sababu Ibilisi amekuwa akitenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili aziangamize kazi za Ibilisi"* (1 Yohana 3:8).

**3. Kuhesabiwa haki**
Wakati mtu anapookolewa na kukombolewa kwa njiya ya damu ya Kristo, amehesabiwa haki mbele ya Mungu, amekubaliwa machoni pake. "*Alifanya hivyo ili kuonyesha haki Yake wakati huu, ili Yeye awe mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yule anayemwamini Yesu*" (Warumi 3:24). "*Kwa kumpitia Yeye (Yesu Kristo), kila mtu amwaminiye anahesabiwa haki kwa kila kitu ambacho asingeweza kuhesabiwa haki kwa sheria ya Musa*" (Matendo 13:39).
Soma tena Warumi 5:1,9 ; 1 Wakorintho 6:11, Tito 3:7.

**4. Upatanisho.**
Neno hili lina maana halisi ifuatayo: "matengenezo ya mkataba kati ya maadui". Mtu anapotenda dhambi ya kwanza, ametengwa, anakuwa mbali na Mungu, inakuwa ni adui wa Mungu. Wakati mtu anapo okolewa, hukombolewa, huhesabiwa haki katika Kristo na badaye hupatanishwa na Mungu, humrudia Mungu, hurejeshwa katika neema ya kimungu. "*Hapo kwanza ninyi mlikuwa mmetengana na Mungu na mlikuwa adui zake katika nia zenu kwa sababu ya mwenendo wenu mbaya. Lakini sasa Mungu <u>amewapatanisha ninyi</u> kwa njia ya mwili wa Kristo kwa kupitia mauti, ili awalete mbele Zake mkiwa watakatifu, bila taka wala lawama*" (Wakolosai 1:21, 22). "*Haya yote yanatokana na Mungu, ambaye ametupatanisha sisi na nafsi yake kwa njia ya Yesu Kristo na kutupatia sisi huduma ya upatanisho*" (2 Wakorintho 5:18). Soma Waefeso 2:16,17.

**5. Msamaha.**
Kwa kuwa mwadilifu (kuhesabiwa haki) mbele za Mungu, ni lazima mtu asamehewe, maana yake ni lazima kupata ondoleo la dhambi zote ametenda dhidi ya Mwenyezi Mungu. Baada ya kupata msamaha wa dhambi, au ondoleo la dhambi, zote zimesahauliwa hata mtu huyu huonekana machoni pa Mungu kama hajawahi kuzitenda kamwe. Ni kwa damu ya Kristo tu ndiko Mungu husamehe makosa yote dhidi ya sheria zake. "*Katika Yeye tunao ukombozi kwa njia ya damu Yake, yaani, msamaha wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema Yake*" (Waefeso

76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.
Tel : +243813148619
+243853163500
Email : klk.bukavu@yahoo.fr

1:7). "*Petro akawajibu, "Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu abatizwe kwa jina la Yesu Kristo, ili mpate kusamehewa dhambi zenu*" (Matendo 2:38).

Soma tena, 26:18 Waefeso 4:32 Wakolosai 1:14, 3:13, 1 Yohana 1:09, 2:12. Tazama pia Mathayo 26:28, Luka 1:77 na Waebrania 9:22.

**6. Kusafishwa**

Kama vile matope wala mafuta huchafua nguo wala mwili, vivyohivyo hambi huchafua roho ya yule anayeitenda. Kwa uchafu wa mwili na mavazi, tunatumiya maji na sabuni. Bali kwa uchafu wa roho, ni damu ya Yesu Kristo tu inayoweza kusafisha nafsi zetu kutokana na uchafu wa dhambi. "*Lakini tukienenda nuruni, kama Yeye alivyo nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu, Mwana Wake yatusafisha dhambi zote*" (1 Yohana 1:7). Soma 1 Wakorintho 6:11, Ufunuo 7:14.

**7. Uponyaji.**

Dhambi imeelezwa pia katika Biblia kama ugonjwa ambao huathiri (huvamia) nafsi ya binadamu. Yesu Kristo ndiye (thabibu) Daktari Mkuu ambaye ana uwezo wa tiba dhidi ya ugonjwa wa kutisha kuliko magonjwa mengine yote. Ni vizuri kusoma kwa makini Mathayo 9:10-13. Fikiria maelezo ya unabii wa uwezo wa Bwana wetu wa kuponya wenye dhambi. "*Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu iliyotuletea sisi amani ilikuwa juu yake, na <u>kwa majeraha yake sisi tumepona</u>*" (Isaya 53:5).

Kuinua huu uwezo wa Mungu uokowao, ukombowao, uhesabiyao haki, upatanishao, usameheao, utakasao na uponyao kwa njiya ya damu ya Yesu Kristo; ni kuinua vilevile neema ya kiMungu maana yote afanyayo Kristo kwa ajili ya wenye dhambi inajumlisha neema ya Mungu bila hiyo watu wasingeliokolewa kutoka dhambi zao. "*Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa kwa neema. Mungu alitufufua pamoja na Kristo na kutuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, ili katika ule ulimwengu ujao apate kuonyesha wingi wa neema Yake isiyopimika, iliyodhihirishwa kwetu kwa wema Wake ndani ya Kristo Yesu"* (Waefeso 2:4-7). Soma Matendo 20:32, Warumi 3:24, Tito 2:11, 3:07, Waebrania 2:09.

***Haya yote, ni kwa neema ya Mungu wala si kwa kazi zetu njema.***

Neno "neema" lina wazo la baraka inayotolewa kwa wale wasio stahili; kwa ufafanuzi mwingine, ni zawadi isiyostahiliwa na mhusika. Hakuna mwenye dhambi awaye yeyote inayestahili haki na wokovu; kinyume chake, kila mumoja alistahili kupoteya milele (Warumi 1: 32). Aidha, mwenye dhambi hawezi kufanya lolote ili kuondoleya nafsi yake hatia na upotovu wa dhambi; hakuna atakalolitenda ili Mungu amkubali. Hata hivyo, Baba wa Mbinguni, mwenye upendo na huruma alimtuma Mwana wake kufa msalabani ili kutoa wokovu kwa wote waliohukumiwa na dhambi. Hivyo, wakati mtu anapokubali wokovu kwa njia ya dhabihu ya Yesu, anapokombolewa kwa damu yake ya thamani kubwa, hupata

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

kitu asichostahili kwa nguvu na wema wake bali kwa kipawa cha neema (zawadi asiyostahili) ya Bwana (Waefeso 2:7). Angalia Warumi 6:23.

Kwa kuwa Yesu Kristo alijitolea kwa hiari yake ili kutimiza mapenzi ya Baba kwa kuacha nafasi ya juu sana yenye sifa na baraka na kukubali kuchangiya shida na mateso ya maisha ya binadamu, na kwa sababu, kwa njia ya mateso yake na kifo, alifanya njiya kwa mwanadamu ili afunguliwe na dhambi zake, ndiyo maana inajulikana kuwa ni neema ya Bwana wetu Yesu Kristo. Ndipo ni kwa neema ya Bwana Yesu tu ndipo sisi tunaamini kuokolewa … (Matendo 15:11). Soma 2 Wakorintho 8:9.

Tunakiri kuwa "**Yesu Kristo peke yake ndilo tumaini kwa ulimwengu**"**!** Ikiwa tunataka kuokolewa toka dhambi zetu na kutarajia nafasi katika ufalme wa milele wa Mungu, ni lazima tuhakikishe kwamba ni kwa njia ya Yesu Kristo tu, na damu yake ndipo tunaweza kufika kwa Mungu. Soma Yohana 14:6. Lakini kama hatuujali wokovu mkuu huu, sisi tutapoteza nafsi zetu hata milele. "*Kwa hiyo, imetupasa kuwa waangalifu sana kuhusu kile tulichosikia, ili tusije tukakiacha. Kwa kuwa ujumbe ulionenwa na malaika ulikuwa imara na kila uasi na kutokutii kulipata adhabu ya haki, je, sisi tutapaje kutapona kama tusipojali wokovu mkuu namna hii? Wokovu huu, ambao mwanzo ulitangazwa na Bwana, kisha ukathibitishwa kwetu na wale waliomsikia.*" (Waebrania 2:1-3).

Ninachagua kumfuata Kristo peke yake na kumsikiliza maana yeye ndiye Njiya, Kweli na Uzima.

Somo la kufuata, la tatu, litatufunza kuhusu mamlaka ya kipekee ya Kristo na kwamba ameyapewa na Mungu wala si kinginen kuimbe chochote. Basi, ikiwa tunataka tufanye mapenzi ya Mungu, tumsikilize Kristo peke yake na kutii maagizo yake wala si ya wanadamu na dhehebu.

**Ikiwa una maswali yoyote wala kutaka mwangaza wa zaidi,**

✍Andikiya:

- Kanisa la kristo pa Bukavu, SLP/Po Box: 222, Cyangugu-Rwanda.
- Email: klk.bukavu@yahoo.fr

⇨ Kutana na watumishi wa Mungu pahali wanaposhiriki pamoja na kanisa kwenye anuani ifuatayo:
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – DRC.